**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**

# MUHTASARI WA MAFUNZO YA UALIMU WA ELIMU YA MSINGI NGAZI YA CHETI

## STADI ZA KAZI

**2009**

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi 2009

ISBN …………………………………………..

Umebuniwa na kutayarishwa na:
Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar-es-Salaam.
Tanzania

Simu: +255 222 773006, 2774420
Faksi: +255 222 774420
Barua pepe: director.tie@tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kutafsiri, kunakili, kupiga chapa au kuutoa muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

## IDHINI

Kozi ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti ni ya miaka miwili na imekusudiwa kuandaa walimu mahiri wenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati. Walimu hao watafundisha katika shule za msingi. Mwalimu mwanafunzi atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhudhuria na kufaulu kozi ya cheti ya miaka miwili ambamo pia atafanya na kufaulu mazoezi ya kufundisha.

Andiko hili linaidhinishwa kuwa ni **Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti- Stadi za Kazi** wa mwaka 2009.

Umeidhinishwa na .......................................................

Saini...................................................................................

Tarehe....................................................................2009

**Kamishna wa Elimu**
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi
S.L.P. 9121
**Dar-es-Salaam**

**Simu: +255 222 110150,110179, 110146**
**Nukushi: +255 222 113271**
**Tovuti: www.moe.go.tz**

## YALIYOMO

UTANGULIZI

Maelezo kuhusu Muhtasari huu ……………………….………………............................… v

Madhumuni ya Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti ……………….............................….. vi

Malengo ya Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti………………..........................……… vi

Ujuzi wa Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti …………………….........................…….. vi

Muundo wa Muhtasari ……………………………………......................……… vii

Upimaji na Tathmini ……………………………………......................…………....viii

Muda wa Mafunzo ……………………………………...................………….......... viii

SEHEMU YA KWANZA: TAALUMA

Malengo …………………………………………………………………….……………1

Ujuzi ……………………………………………………………………………………….1

**Mada**

1. Usanii wa Picha Chapa Maumbo na Mapambo ……………….................………....2
2. Ususi …………………………………………………………………….………6
3. Sanaa za Maonyesho …………………………………………………..…………7
4. Ushoni wa Nguo ……………………………………………………….………….10
5. Muziki ……………………………………………………………….…………….12
6. Kilimo, Ufugaji na Uvuvi ……………………………………………….…..…..13
7. Upishi ……………………………………………………………………….………..15
8. Udobi ………………………………………………………………………………16
9. Upigaji Picha ……………………………………………………………….………18
10. Biashara Ndogo Ndogo ……………………………………………..……………20
11. Ufundi ………………………………………………………………..….………….21

SEHEMU YA PILI: UFUNDISHAJI

Malengo ……………………………………………………………..…………………..24

Ujuzi ………………………………………………………………..…………………...24

**Mada**

1. Misingi ya Kufundisha somo la Stadi za Kazi ……………...........………........…25
2. Maandalizi ya ufundishaji ………………………………………….………………30

3. Ufundishaji ……………………………………………………………………......33
4. Upimaji ………………………………………………………….……………… 46
5. Rejea ……………………………………………………………….………..…50

# UTANGULIZI

## Maelezo Kuhusu Muhtasari wa Somo

Muhtasari huu umeboreshwa ili kuchukua nafasi ya Muhtasari wa Ngazi ya Cheti wa mwaka 2003. Muhtasari huu umekusudiwa kumwezesha mwanachuo kujenga ujuzi wa kufundisha somo la Stadi za Kazi katika shule za msingi na pia kumjenga kitaaluma na kitaalamu katika somo hili.

Muhtasari wa mwaka 2008 umetilia mkazo nyanja ya ufundishaji na taaluma tofauti na ule wa mwaka 2003 ambao haukubainisha wazi maudhui ya taaluma, badala yake ulitilia mkazo zaidi katika ufundishaji tu. Aidha, muhtasari unasisitiza ufundishaji na ujifunzaji shirikishi unaomwezesha mwanachuo kuwa na fursa kubwa ya kufikiri na kutenda katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Ili kumsaidia Mkufunzi yametolewa mapendekezo ya mbinu za kufundishia na kujifunzia, zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia pamoja na upimaji. Mkufunzi anahimizwa kutumia mbinu mbalimbali, zana zinazopatikana katika mazingira husika na upimaji alioshauriwa kwenye muhtasari huu. Pamoja na mbinu zilizoainishwa mkufunzi anaweza kutumia mbinu nyinginezo kulingana na mahitaji ya mada anayofundisha.

## Sababu za Kuboresha Muhtasari

Miongoni mwa malengo ya Mpango wa Elimu ya Msingi (MMEM) ni kuwa na walimu bora kitaalamu na kitaaluma. Hali kadhalika Dira ya Elimu ya Mafunzo inasisitiza uwepo wa walimu walio bora kitaaluma na katika mbinu za kufundishia na kujifunzia ili kukabiliana na changamoto za mahitaji na matarajio ya kielimu katika milenia hii. Mwelekeo wa dira na mpango wa elimu kwa ujumla ni kuandaa walimu wenye ujuzi wa kufundisha masomo ya elimu ya msingi kwa kuzingatia misingi, kanuni na mielekeo inayopasa. Walimu wa Stadi za Kazi wanahitaji kupata ujuzi wa kuweza kuyatumia vema mazingira yao katika kuwezesha somo hilo kufanikiwa kwa hiyo muhtasari huu umeandaliwa ili kukidhi mahitaji yote yaliyotajwa hapo juu na kumwezesha mwalimu kulimudu vema somo la Stadi za Kazi.

**Madhumuni ya Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti**

Mwishoni mwa mafunzo ya ualimu ya miaka miwili (2) mwanachuo aweze:

a) Kutafsiri Mtaala wa Elimu ya Msingi na Mihtasari yake katika masomo darasani.
b) Kuandaa na kutumia mbinu shirikishi katika ufundishaji/ujifunzaji wa wanafunzi katika shule za msingi.
c) Kubuni, kuendeleza na kufaragua nyenzo za kufundishia na kujifunzia katika elimu ya msingi.
d) Kufanya utafiti kuhusu wanafunzi ili kuwabaini na kuwasaidia wale wenye mahitaji maalumu katika shule za msingi.
e) Kurithisha desturi, maadili na tabia zinazokubalika kwa wanafunzi wa shule za msingi.
f) Kuchagua, kupanga, kusimamia na kuongoza vipindi darasani katika shule za msingi.
g) Kufundisha kwa ufanisi masuala mtabuko.
h) Kutunga majaribio na mitihani inayoendana na mtaala wa elimu ya msingi kwa kuzingatia nyanja zote tatu za kujifunza.

**Ujuzi wa Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti**

Mwishoni mwa mafunzo ya miaka miwili (2) mwanachuo awe na uwezo wa:

a) Kubaini, kushauri na kunasihi wanafunzi wenye mahitaji mbalimbali maalumu kwa kuzingatia mazingira jumuishi.
b) Kukuza maendeleo ya kihaiba, kiakili na tabia za kimaumbile kwa wanafunzi wa shule za Msingi.
c) Kutumia stadi mbalimbali, maarifa ya kiteknolojia na ubunifu katika ufundishaji.
d) Kupima na kutathmini maendeleo ya wanafunzi kitaaluma na kitabia.
e) Kutumia stadi za kiuongozi na kiutawala kuweka ulinzi na usalama kwa wanafunzi wa shule za msingi.
f) Kufanya tafiti ndogo ndogo kuhusu maendeleo ya wanafunzi katika kujifunza.
g) Kubuni, kutengeneza na kutumia zana katika kufundisha na kujifunza.
h) Kutafuta maarifa na stadi katika kujiendeleza kitaalamu.
i) Kumudu maudhui ya mada za masomo atakayofundisha.
j) Kubainisha, kutafsiri na kufundisha masuala mtambuko kwa ufanisi.

**Malengo ya Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti**

a) Kukuza uelewa wa wanachuo katika nadharia za kielimu, kanuni, utafiti, misingi ya mitaala na utendaji.
b) Kuendeleza uwezo wa mwanachuo kumudu masomo ya taaluma, ufundishaji, teknolojia na ubunifu.
c) Kumwezesha mwanachuo kukuza mbinu za kusimamia uongozi na utawala wa darasa.
d) Kutoa nafasi kwa wanachuo kuweza kujiongezea maarifa na ujuzi katika ushauri nasaha, elimu maalumu na masuala mtambuko.
e) Kuandaa walimu wenye stadi na mbinu za utafiti, upimaji na tathmini.

**Madhumuni ya Kufundisha Somo la Stadi za Kazi**

Kuandaa walimu wenye maarifa na stadi za kutosha kufundisha somo la Stadi za Kazi katika shule za msingi.

**Muundo wa Muhtasari**

Muhtasari umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni maudhui ya taaluma ambayo yamebainisha mada zitakazofundishwa ili kumjenga mwanachuo kitaaluma. Sehemu ya pili ni ile ya ufundishaji ambayo imebeba mada zinazolenga kumjengea mwanachuo uwezo wa kufundisha mada zilizopo kwenye muhtasari wa Stadi za Kazi kwa shule za msingi.

Katika ufundishaji, mada zilizozingatiwa ni **misingi ya kufundisha somo la Stadi za Kazi, maandalizi ya ufundishaji, ufundishaji na upimaji na tathmini**. Mada kumi na moja zimeteuliwa ili kumwezesha mwanachuo kuzifundisha ipasavyo. Mada hizo ni:
Usanii wa Picha Chapa Maumbo na Mapambo, Ususi, Sanaa za Maonyesho, Ushoni wa Nguo, Muziki, Kilimo, Ufugaji na Uvuvi, Upishi, Udobi, Upigaji Picha, Biashara Ndogo Ndogo na Ufundi.

**Upimaji na Tathmini**

Muhtasari huu umependekeza mbinu mbalimbali za upimaji na tathmini zitakazotumika wakati wa mchakato wa ujifunzaji wa kozi ya ualimu. Upimaji tamati utafanywa na baraza la mitihani na utakuwa na alama 50. Upimaji endelevu utafanywa na mkufunzi wakati mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unaendelea na utakuwa na alama 50. Upimaji huu unahusisha mazoezi, majaribio, mkoba wa kazi, ufundishaji kiduchu na ushiriki katika kazi za darasani. Uzito wa kila aina ya upimaji umeonyeshwa katika jedwali lifuatalo.

Jedwali la Upimaji Endelevu na Tamati

| **Vipengele** | **Mbinu za upimaji** | **Mwaka** | | | | **Idadi** | **Alama (%)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Mwaka I** | | **Mwaka II** | | | |
| | | **Muhula I** | **Muhula II** | **Muhula I** | **Muhula II** | | |
| Taaluma | Majaribio | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 5% |
| | Kazi mradi | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 5% |
| | Kazi ya kila mwanachuo | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 5% |
| Ufundishaji | Majaribio | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 5% |
| | Mkoba wa kazi | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 5% |
| | Uandishi wa Insha | 1 | 1 | 1 | 1 | 4 | 5% |
| Mitihani ya mwisho wa muhula | Taaluma na Ufundishaji | 1 | 1 | 1 | | 3 | 20% |
| Upimaji Endelevu | | | | | | | 50% |
| Mtihani wa Baraza la Mitihani la Taifa | | - | - | - | | 1 | 50% |
| Jumla ya Alama za Upimaji Endelevu na Tamati | | | | | | | 100% |

**Muda wa Mafunzo**

Muhtasari wa somo la Stadi za Kazi umekusudiwa kukamilishwa kwa kipindi cha miaka miwili. Mtazamo wa somo hili ni kumjengea mwanachuo misingi muhimu ya Stadi za Kazi katika jamii

zitakazomwezesha kufundisha kikamilifu somo hili katika elimu ya msingi. Maswala mtambuko yamezingatiwa katika maudhui pamoja na watoto wenye mahitaji maalum. Mada kuu zimegawanywa katika mada ndogo ndogo ambazo zimetolewa malengo mahsusi, njia na mbinu za kufundishia na kujifunzia pamoja na vifaa/zana vitakavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo. Kila mada ndogo imeonyesha muda utakaotumika, mkufunzi anashauriwa atumie muda huo vizuri. Somo hili litatumia saa 3 kila wiki. Saa 1 kwa taaluma na saa 2 kwa ufundishaji.

Somo la Stadi za Kazi ni moja kati ya masomo 15 ambayo kila mwanachuo anatarajiwa kuyasoma. Katika sehemu ya taaluma mwanachuo anatarajiwa kujenga ujuzi katika mada ndogo zilizoteuliwa ndani ya mada kuu kumi na moja.

## SEHEMU YA KWANZA: TAALUMA

### Ujuzi wa Somo

Baada ya kukamilisha mafunzo ya miaka miwili mwanachuo aweze:-

a) Kutumia misingi ya somo la Stadi za Kazi kufundisha somo kikamilifu.
b) Kuelewa umuhimu wa kufundisha somo la Stadi za Kazi.
c) Kufundisha kwa ufanisi mada zote za Stadi za Kazi.
d) Kuchopeka masuala mtambuko katika mada mbalimbali za Stadi za Kazi.

### Malengo ya Somo

Baada ya mafunzo ya miaka miwili mwanachuo aweze:-

a) Kujijengea maarifa, stadi na mielekeo ya Stadi za Kazi.
b) Kumjengea mwanafunzi wa Elimu ya Msingi tabia ya kutumia muda wake wa ziada kwa manufaa.
c) Kutumia misingi ya stadi za ujasiriamali katika kufundisha Elimu ya Msingi.
d) Kuzingatia masuala mtambuko na mahitaji maalum katika kazi za Stadi za Kazi.
e) Kubuni, kutengeneza, kufaragua vifaa vya kufundishia/kujifunzia Stadi za Kazi na kuvitumia.

## 1.0 USANII WA PICHA , CHAPA, MAUMBO NA MAPAMBO

### 1.1 Uchoraji wa Picha kwa Kutumia Vigezo

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kutengeneza vigezo
b) Kupanga vizuri vigezo kwa kuzingatia maumbo ya picha atakayochora
c) Kuchora picha kwa kutumia vigezo.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Onyesho mbinu kuonyesha jinsi ya kuchora picha kwa kutumia vigezo
b) Kazi mradi kuchora vigezo.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Karatasi ngumu, mkasi au visu vya kukatia karatasi, rula, penseli, ubao wa kukatia.
b) Picha zitakazochorwa
c) Sampuli za vigezo.

**Upimaji**

a) Fomu ya uchunguzi kupima usahihi wa kutengeneza vigezo
b) Majaribio
c) Mazoezi.

### 1.2 Utengenezaji wa Picha kwa Kubandika Makunzi Mbalimbali

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya kutengeneza picha
b) Kukusanya makunzi yanayofaa kutengenezea picha
c) Kutengeneza picha kwa kutumia makunzi ya aina mbalimbali.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo
b) Onyesho mbinu kuonesha namna ya kutengeneza picha kwa kutumia makunzi ya aina mbalimbali
c) Kazi mradi kutengeneza picha.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Karatasi ngumu, mikasi/visu vya kukatia karatasi, gundi ya mbao.
b) Makunzi ya aina mbalimbali.

**Upimaji**

a) Mazoezi
b) Kazi mradi kutengeneza picha kwa kutumia makunzi ya aina mbalimbali
c) Fomu ya uchunguzi kuangalia utengenezaji wa picha

**1.3 Usanii wa Picha za Rangi za Maji**

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha tabia za rangi za maji
b) Kuandaa vifaa vinavyotumika katika usanii wa picha kwa rangi za maji
c) Kusanii picha za rangi za maji hatua kwa hatua.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Fikiri, jozisha shirikisha
b) Onyesho mbinu kuonesha usanii wa picha kwa rangi za maji
c) Majadiliano
d) Kazi mradi kusanii picha za rangi za maji.

**Vifaa/zana za kufundishia/kujifunzia**

a) Rangi za maji hasa za msingi, paleti, brashi kubwa na ndogo, karatasi nzito manila nyeupe,
b) Sampuli za picha zilizosanifiwa kwa rangi za maji
c) Maji na vyombo vya kuwekea maji.

**Upimaji**

a) Mazoezi
b) Majaribio

**1.4 Upambaji wa Nguo kwa Mtindo wa Batiki**

**Muda: Saa 3**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza mchakato wa namna ya kupamba nguo kwa mtindo wa batiki
b) Kubainisha vifaa na kemikali zinazotumika katika kupamba batiki
c) Kupamba nguo kwa mtindo wa batiki hatua kwa hatua
d) Kunadhifisha na kuhifadhi vyema nguo zilizopambwa.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo
b) Majadiliano
c) Kualika mtaalamu kuelekeza jinsi ya kupamba nguo kwa mtindo wa batiki.
d) Onyesho mbinu kuonesha namna ya kupamba nguo kwa mtindo wa batiki.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Kemikali (sodium na caustic soda), mshumaa, rangi za nguo, sabuni, maji
b) Vitambaa vya pamba, sampuli za vitambaa vya batiki.
c) Vifaa vya kuchemshia (pipa au sufuria), vifaa vya kuchanganyia rangi (masinia ya plastiki), karai, mwiko, jiko lenye moto, pasi na kamba ya kuanikia nguo, meza,

kifaa cha kuzuia kusambaa kwa kemikali kama vile nailoni, majani ya mgomba au mabati, glovu na kimori cha nailoni, buti

**Upimaji**

a) Insha kuhusu mchakato wa namna ya kupamba nguo kwa mtindo wa batiki
b) Mazoezi na Majaribio.

**1.5 Uchapaji wa picha kwa njia ya kimia**

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza mchakato wa uchapaji kwa njia ya kimia
b) Kuandaa vifaa na mazingira ya kuchapa kwa njia ya kimia
c) Kuchapa kwa njia ya kimia hatua kwa hatua.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Fikiri jozisha shirikisha
b) Majadiliano
c) Onesho mbinu kuonesha uchapaji kwa njia ya kimia
d) Kualika mtaalamu kuonesha mchakato mzima wa uchapaji kwa njia ya kimia
e) Ziara kuona uchapaji kwa kutumia njia ya kimia.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Vibao, wavu, misumari, kisambazio cha rangi, karatasi ya kukatia stenseli, mkasi/visu vya kukatia karatasi, karatasi za kuchapia, pini za kushikilia wavu.
b) Sampuli ya fremu ya kimia na stenseli.

**Upimaji**

a) Insha kuhusu mchakato wa uchapaji kwa njia ya kimia.
b) Kazi mradi kuchapa kwa njia ya kimia.
c) Mazoezi

## 2.0 USUSI

### 2.1 Usukaji Ukili

**Muda Saa 3**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza hatua za kusuka ukili
b) Kuchana chane za ukindu ipasavyo
c) Kusuka ukili wa njia moja hatua kwa hatua
d) Kusuka ukili wa njia mbilihatua kwa hatua

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo
b) Onesho mbinu kuonesha namna ya kuchana chane za ukindu hatua kwa hatua
c) Ziara ya mafunzo kuona kili mbalimbali zinavyosukwa.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Ukindu, kili za njia moja
b) Kisu, shazia, beseni, maji, kasha la kuhifadhia

**Upimaji**

a) Mazoezi.
b) Kazi mradi ya kusuka ukili

### 2.2 Ushonaji wa Vifani

**Muda Saa 1**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza hatua za kushona vifani
b) Kushona kifani cha kofia na kikapu
c) Kunadhifisha vifani vilivyoshonwa.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Onesho mbinu la namna ya kushona vifani
b) Majadiliano

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Kifani cha kofia na kikapu
b) Sindano/shazia
c) Uzi/kamba
d) Kisu

**Upimaji**

a) Mazoezi
b) Kazi mradi ya kushona na kunadhifisha vifani

## 3.0 SANAA ZA MAONESHO

### 3.1 Dhana ya Sanaa za Maonesho

**Muda Saa 1**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana ya sanaa za maonesho
b) Kuaridhia umuhimu wa sanaa za maonesho
c) Kufafanua aina za sanaa za maonesho

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo
b) Majadiliano

**Zana/vifaa vya kufundishai na kujifunzia**

a) Kielelezo cha ramani ya dhana
b) Picha/video za sanaa za maonyesho
c) Vifaa vya sanaa za maonyesho.

**Upimaji**

Majaribio

## 3.2 Uchezaji Ngoma Sahili

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kujadili jinsi ya kucheza ngoma sahili
b) Kubainisha ala za ngoma zitakazochezwa
c) Kupiga ala zinazotumika katika ngoma husika
d) Kucheza ngoma sahili

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Majadiliano
b) Onesho mbinu la namna ya kucheza ngoma
c) Kualika mtaalamu kuonyesha jinsi ya kucheza ngoma.

**Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

Ala mbalimbali za ngoma.

**Upimaji**

Mazoezi

## 3.3 Uigizaji wa Hadithi

**Muda saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kusimulia hadithi
b) Kueleza ujumbe ulioko katika hadithi
c) Kuandaa vifaa vya kuigizia
d) Kuigiza hadithi

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Igizo dhima kuigiza matendo katika hadithi
b) Bungua bongo
c) Majadiliano

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Hadithi mbalimbali
b) Vifaa vitakavyohusika kwenye igizo

**Upimaji**

a) Mazoezi
b) Mkoba wa kazi

## 3.4 Kutunga na Kughani Mashairi

**Muda saa 3**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza kanuni za kutunga mashairi
b) Kutunga mashairi
c) Kughani mashairi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Fikiri jozisha shirikisha
b) Majadiliano
c) Kazi mradi ya kutunga na kughani shairi

**Vifaa/Zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Mashairi yaliyoandikwa
b) Kanda zilizohifadhi mashairi yaliyoghaniwa

**Upimaji**

Mazoezi

## 4.0 USHONAJI WA NGUO

### 4.1 Mishono Sahili

**Muda saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha kazi za mishono sahili
b) Kuchora aina mbalimbali za mishono sahili
c) Kushona mishono sahili mbalimbali.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo
b) Majadiliano
c) Onesho mbinu la namna ya kushona mishono hiyo.

**Vifaa/Zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Sindano za saizi mbalimbali, nyuzi za rangi mbalimbali, subana, gurudumu la kutarizia,
b) Kitambaa,
c) Sampuli za mishono iliyotarizwa.

**Upimaji**

a) Majaribio
b) Mkoba wa kazi

### 4.2 Kutengeneza Vigezo na Kushona

**Muda Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kuchora vigezo kwa vipimo sahihi
b) Kukata vigezo
c) Kushona vigezo hatua kwa hatua.
d) Kushona nguo kwa kutumia vigezo

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo
b) Onesho mbinu la namna ya kuchora, kukata na kushona vigezo na nguo

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Karatasi za kaki au za kawaida, mfuto, mkasi na wembe, mita kamba au rula, sindano na uzi,
b) Sampuli za vigezo, penseli/chaki
c) Nguo zilizoshonwa.

**Upimaji**

a) Majaribio
b) Mkoba wa kazi
c) Kazi mradi ya kushona vigezo na nguo

## 4.3 Utarizi wa Mishono Mbalimbali

**Muda Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kuchora ruwaza za kutariziwa
b) Kutarizi mishono ya aina mbalimbali
c) Kunadhifisha vitu vilivyotarizwa.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Onesho mbinu la namna ya kutarizi mishono mbalimbali
b) Matembezi ya galari kuona na kujadili ubora wa kazi

**Vifaa/Zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Sindano za saizi mbalimbali za kutarizia
b) Nyuzi za rangi mbalimbali za kutarizia
c) Vitambaa vilivyotariziwa na visivyotarizwa.

**Upimaji**

a) Mazoezi.

b) Fomu ya uchunguzi usahihi wa kutarizi

## 5.0 MUZIKI

### 5.1 Uimbaji

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kubaini mbinu za uimbaji

b) Kubaini solfa za muziki na sauti zake

d) Kuimba solfa kwa kufuata hatua mbalimbali

e) Kuimba nyimbo kwa kutumia solfa

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Onesho mbinu la namna ya kuimba

b) Kuimba kwa kuzingatia solfa

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Picha za mikao wakati wa kuimba.

b) Ala za muziki

c) Kinasa sauti

d) Kanda zenye nyimbo

**Upimaji**

a) Mazoezi

b) Fomu ya uchunguzi ya kupima usahihi wa kuimba nyimbo kwa kutumia solfa

**5.2 Upigaji Ala Sahihi za Muziki**

**Muda: saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kuainisha ala sahihi za muziki
b) Kupiga ala halisi za muziki katika kukoleza kwaya
c) Kutunza ala halisi za muziki baada ya kupiga.

**Mbinu za kujifunzia/kufundishia**

a) Majadiliano
b) Onesho mbinu la namna ya kupiga ala sahihi za muziki.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Kanda za kaseti na kinasa sauti
b) Ala halisi za muziki

**Upimaji**

a) Mazoezi
b) Maswali ya mdomo

## 6.0 KILIMO, UFUGAJI NA UVUVI

**6.1 Ustawishaji wa Mboga Mbalimbali**

**Muda: saa 3**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza umuhimu wa mboga
b) Kuainisha makundi ya mboga
c) Kueleza kanuni za ustawishaji wa mboga
d) Kustawisha mboga

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Majadiliano
c) Ziara kuona namna mboga zinavyostawishwa
d) Onesho mbinu la jinsi ya kustawisha mboga

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Majembe, panga, sepetu, keni
b) Samadi, mboji, mbegu za mboga, maji

**Upimaji**

a) Insha kuhusu ustawishaji wa mbinu
b) Kazi mradi ya kustawisha mboga

## 6.2 Ufugaji Bora

**Muda: saa 7**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha kanuni za ufugaji bora wa samaki, nyuki, kuku wa kienyeji na ng'ombe wa maziwa
b) Kueleza faida za ufugaji
c) Kufafanua namna ya kufuga samaki, nyuki, kuku wa kienyeji na ng'ombe wa maziwa

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Majadiliano
c) Kualika mtaalam kueleza namna ya kufuga wanyama hao
d) Ziara mafunzo kuona namna wanyama mbalimbali wanavyofugwa

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Vifaa vinavyohusika na ufugaji huo
b) Picha/video zinazoonesha ufugaji bora

**Upimaji**

Mazoezi na majaribio

## 7.0 UPISHI

### 7.1 Upishi wa Vyakula Mbalimbali

**Muda: saa 6**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza kanuni za upishi
b) Kufafanua faida za upishi
c) Kuainisha njia mbalimbali za upishi wa vyakula
d) Kupika vyakula mbalimbali

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano
b) Onesho mbinu la namna ya kupika vyakula kwa njia mbalimbali.
c) Kualika mtalamu kuonyesha namna ya kupika vyakula mbalimbali
d) Ziara mafunzo kuona upishi wa aina mbalimbali

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Chati inayoonyesha njia mbalimbali za upishi
b) Picha za vyakula mbalimbali
c) Vyakula halisi
d) Vifaa vya kupikia

**Upimaji**

a) Majaribio na mazoezi
b) Fomu ya uchunguzi kuangalia upikaji wa vyakula mbalimbali

**7.2 Utayarishaji wa Juisi za Matunda**

**Muda: saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza umuhimu wa juisi
b) Kubaini matunda yafaayo kutengenezea juisi
c) Kutengeneza juisi kwa njia mbalimbali

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano
b) Bungua bongo
c) Onesho mbinu la j kutengeneza juisi

**Zana za kufundishia/kujifunzia**

a) Matunda ya aina mbalimbali
b) Vyombo vya kutengenezea na kuhifadhia juisi
c) Maji na sukari

**Upimaji**

a) Mazoezi
b) Fomu ya uchunguzi kuangalia utengenezaji wa juisi

## 8.0 UDOBI

**8.1 Ufuaji wa nguo**

**Muda: saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza faida za ufuaji wa nguo
b) Kuainisha kanuni za ufuaji wa nguo za aina mbalimbali
c) Kufua nguo za aina mbalimbali kwa kufuata kanuni

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano

b) Maswali na majibu

c) Onesho mbinu la kufua nguo za aina mbalimbali kwa kufuata kanuni

**Zana/vifaa v ya kufundishia na kujifunzia**

a) Nguo za aina mbalimbali

b) Sabuni, maji, ndoo, beseni, meza, vibanio na kamba ya kuanikia nguo

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo

b) Fomu ya uchunguzi kuangalia ufuaji wa nguo

**8.2 Upigaji Nguo Pasi**

**Muda: saa 1**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza faida za kupiga nguo pasi.

b) Kuonyesha hatua za kupiga nguo pasi

c) Kupiga pasi nguo za aina mbalimbali

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano

b) Onesho mbinu la namna ya kupiga nguo pasi

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Pasi, tandiko la kupigia pasi

b) Nguo za aina mbalimbali

c) Maji na moto

**Upimaji**

a) Majaribio

b) Orodha kaguzi kuangalia upigaji pasi nguo

## 9.0 UPIGAJI PICHA

### 9.1 Kamera

**Muda: saa 1**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya kamera

b) Kubainisha sehemu mbalimbali za kamera

c) Kufafanua kazi za kila sehemu ya kamera

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali na majibu

b) Majadiliano

**Vifaa/zana za kufundishia/kujifunzia**

a) Kamera

b) Picha/chati za vifaa vya kamera na kazi zake

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo

b) Mazoezi

### 9.2 Upigaji Picha Tuli

**Muda: saa 1**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kufafanua faida za upigaji picha

b) Kueleza kanuni za kupiga picha tuli

c) Kupiga picha tuli kwa kuzingatia kanuni hizo

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Majadiliano
c) Onyesho mbinu la jinsi ya kupiga picha tuli

**Vifaa/Zana za Kufundishia/kujifunzia**

a) Kamera
b) Bango lenye kanuni za upigaji picha tuli
c) Vielelezo vya namna ya kupiga picha tuli
d) Picha zilizopigwa

**Upimaji**

a) Majaribio
b) Orodha hakiki kupima uwezo kupiga picha tuli

**9.3 Utunzaji wa Kamera, Negativu na Picha**

**Muda: saa 1**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza mambo ya kuzingatia katika kutunza kamera, negativu na picha
b) Kubainisha vifaa vinavyotumika kutunza kamera, negativu na picha
c) Kuigiza namna ya kutunza kamera, negativu na picha

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo
b) Onyesha mbinu la namnaya kutunza kamera, negativu na picha
c) Majadiliano

**Vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Kamera, negativu na picha

b) Vifaa vya kuhifadhia kamera, negativu na picha

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo

b) Mazoezi

## 10.0 BIASHARA NDOGO NDOGO

### 10.1 Dhana ya biashara ndogo ndogo.

**Muda: saa 1**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza dhana ya biashara ndogondogo

b) Kufafanua aina za biashara ndogondogo

c) Kueleza faida za biashara ndogondogo

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo

b) Majadiliano

c) Ziara ya mafunzo kuona uendeshaji wa biashara ndogondogo

**Vifaa/zana za kufundishia/kujifunzia**

Picha zinaoonesha shughuli za biashara ndogo ndogo

**Upimaji**

a) Insha kuhusu dhana aina na faida za biashara ndogondogo

b) Ripoti ya ziara

## 10.2 Uanzishaji na Uendeshaji wa Biashara Ndogo Ndogo

**Muda: saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza mambo muhimu katika kuanzisha biashara ndogondogo
b) Kufafanua hatua za kuendesha biashra ndogondogo
c) Kuanzisha biashara ndogo ndogo

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano
b) Ziara mafunzo kutembelea biashara ndogo ndogo
c) Kualika mtaalamu kueleza kanuni za kuendesha biashara ndogondogo

**Zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia**

a) Daftari la kutunza mahesabu
b) Daftari la kutunza bidhaa
c) Sampuli ya leseni
d) Mchanganua wa biashara ndogo ndogo.

**Upimaji**

a) Insha kuhusu uanzishaji na uendeshaji wa biashara ndogo ndogo
b) Maswali ya mdomo

# 11.0 UFUNDI

## 11.1 Matengenezo ya Baiskeli

**Muda: saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada hii mwanachuo aweze:-

a) Kuaridhia sehemu za baiskeli na kazi zake
b) Kueleza aina ya matengenezo yanayotakiwa katka baiskeli na gharama zake

c) Kuainisha vifaa vitakavyotakiwa kufanya matengenezo ya baiskeli
d) Kufanya matengenezo

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Kualika fundi wa baiskeli kufundisha namna kufanya matengenezo ya baiskeli
b) Ziara mafunzo kuona matengenezo ya baiskeli
c) Onesho mbinu la matengenezo ya baiskeli
d) Majadiliano

**Vifaa /zana za kufundishia /kujifunzia**

a) Baiskeli iliyoharibika.
b) Vifaa vya kufanyia matengenezo ya baiskeli.
c) Kisanduku cha huduma ya kwanza.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo
b) Fomu ya uchunguza kuangalia matengenezo ya baiskeli.

**11.2 Matengenezo ya Viatu**

**Muda: saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilika mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha vifaa vinavyotakiwa katika matengenezo ya viatu na gharama zake
b) Kueleza hatua za kufanya matengenezo ya viatu
c) Kufanya matengenezo ya viatu

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano
b) Onesho mbinu la namna ya kufanya matengenezo ya viatu
c) Ziara ya kuona matengenezo ya viatu

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Viatu vilivyoharibika
b) Uzi wa kushonea viatu, vipande vya ngozi, gundi ya viatu, soli ya kiatu
c) Nyundo, misumari, kisu, nta na sabuni, orodha ya bei za

**Upimaji**

a) Majaribio
b) Fomu ya uchunguzi kuangalia matengenezo ya viatu

## SEHEMU YA PILI: UFUNDISHAJI

### Ujuzi wa Somo

Baada ya kujifunza somo hili mwanachuo anatarajiwa kupata ujuzi ufuatao:

a) Kuelewa umuhimu wa kujifunza somo la Stadi za Kazi.

b) Kutenda fani za Stadi za Kazi kiustadi.

c) Kufundisha somo la Stadi za Kazi.

d) Kuzingatia utunzaji wa mazingira na mahitaji maalumu wakati anapofundisha Stadi za Kazi.

### Malengo ya Somo

Baada ya mafunzo ya miaka miwili mwanachuo aweze:-

a) Kujenga stadi, maarifa na mwelekeo wa msingi katika Stadi za Kazi.

b) Kutumia mbinu mbalimbali za kufundishia/kujifunzia somo la Stadi za Kazi.

c) Kupenda na kuendeleza somo la Stadi za Kazi.

d) Kuzingatia masuala mtambuko na mahitaji maalumu katika kazi za Stadi za Kazi.

e) Kubuni, kutengeneza na kufaragua vifaa vya kufundishia/kujifunzia na kuvitumia.

## 1.0 MISINGI YA UFUNDISHAJI STADI ZA KAZI.

### 1.1 Urasini wa Ujumi

**Muda: Saa 1**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kufasili msingi wa urasini wa ujumi
b) Kueleza umuhimu wa msingi wa urasini wa ujumi katika kufundisha Stadi za Kazi
c) Kutumia msingi huu katika kufundisha na kujifunza Stadi za Kazi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Majadiliano
c) Onesho mbinu kuonyesha namna ya kutumia msingi huu katika kufundisha somo.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Picha mbalimbali zenye kuvutia
b) Kazi za ufundi zilizosanifiwa.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo
b) Mazoezi

### 1.2 Kuendeleza Ubunifu, Uundaji, Utungaji na Ufaraguzi

**Muda: Saa 1**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kufasili msingi wa kuendeleza ubunifu, uundaji, utungaji na ufaraguzi
b) Kubaini umuhimu wa msingi huu katika kufundisha somo la Stadi za Kazi
c) Kufundisha mada za Stadi za Kazi kwa kutumia msingi huu.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Kualika mtaalamu kueleza jinsi ya kufundisha kwa kutumia msingi huo
b) Onyesho la namna ya kufundisha kwa kutumia msingi huo.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Kazi mbalimbali za sanaa za picha
b) Kazi mbalimbali za sanaa za maonyesho
c) Kazi mbalimbali za upishi
d) Kazi mbalimbali za sanaa za ufundi.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo
b) Majaribio
c) Kazi mradi za kupima welewa wa mwanachuo kutumia msingi huo kufundisha somo la Stadi za Kazi ipasavyo.

### 1.3 Utendaji, Umakini na Udadisi katika Ufundishaji na Ujifunzaji.

**Muda: Saa 1**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kufasili msingi wa utendaji, umakini na udadisi
b) Kueleza umuhimu wa msingi huu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kazi
c) Kutumia msingi huo katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kazi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Fikiri jozisha shirikisha
b) Majadiliano

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Kazi nzuri za Stadi za Kazi zilizonadhifishwa
b) Picha za kazi za Stadi za Kazi.

**Upimaji**

a) Mazoezi
b) Majaribio

## 1.4 Weledi wa Matumizi na Uhifadhi wa Mazingira na Jamii yake.

**Muda: Saa 1**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kufasili msingi wa weledi wa matumizi na uhifadhi wa mazingira
b) Kueleza umuhimu wa msingi huu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kazi
c) Kutumia msingi huu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kazi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Fikiri jozisha shirikiana
b) Majadiliano kueleza

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Mazingira halisi
b) Picha zinazoonyesha uhifadhi wa mazingira
c) Picha zinazoonyesha ushirikiano wa jamii

**Upimaji**

a) Orodha hakiki ya kupima uwezo wa mwanachuo katika kufundisha kwa kuzingatia msingi huu.
b) Kazi mradi ya kupima uelewa wa wanachuo kutumia msingi huu kikamilifu katika kazi mbalimbali za Stadi za Kazi.

## 1.5 Usafi, Mpangilio, Uadilifu na Usalama katika Utendaji Kazi.

**Muda: Saa 1**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kufasili msingi wa usafi, mpangilio, uadilifu na usalama
b) Kueleza umuhumu wa kutumia kanuni hii katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kazi
c) Kutumia msingi huu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kazi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Fikiri jozisha shirikisha
b) Majadiliano

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

Kazi nzuri za Stadi za Kazi zilizondaliwa na kuzingatia msingi huu.

**Upimaji**

Orodha hakiki ya kupima uwezo wa mwanachuo wa kufundisha kwa kuzingatia msingi huu.

## 1.6 Utambuzi, Usikivu, Vionjo na Hisia

**Muda: Saa 1**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kufasili msingi wa utambuzi, usikivu, vionjo na hisia
b) Kueleza umuhimu wa msingi huu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kazi
c) Kutumia msingi huu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kazi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Fikiri jozisha shirikiana
b) Majadiliano.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

Kazi nzuri za Stadi za Kazi zenye mwelekeo wa uimbaji kama vile nyimbo, ushairi, maghani na melodia.

**Upimaji**

Orodha hakiki ya kupima uwezo wa mwanachuo wa kufundisha kwa kutumia msingi huu.

## 1.7 Kuzingatia Urari wa Kijinsia katika Mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji

**Muda: Saa 1**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kufasili msingi wa urari wa kijinsia katika ufundishaji na ujifunzaji
b) Kueleza umuhimu wa msingi huu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kazi
c) Kutumia msingi huu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kazi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Fikiri jozisha shirikisha
b) Majadiliano

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

Picha zenye kuonyesha shughuli mbalimbali zikifanywa baina ya wanawake na wanaume kwa pamoja.

**Upimaji**

Orodha hakiki ya kupima uwezo wa mwanachuo wa kufundisha kwa kutumia msingi huu.

## 2.0 MAANDALIZI YA UFUNDISHAJI

### 2.1 Uchambuzi wa Muhtasari

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza sababu za kuchambua muhtasari.
b) Kufasili vipengele vinavyounda kila sehemu ya muhtasari.
c) Kuchambua muundo wa muhtasari.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo
b) Maswali na majibu kubaini vipengele vya muhtasari.
c) Onesho mbinu kuupitia muhtasari hatua kwa hatua.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

Muhtasari wa Stadi za Kazi

**Upimaji**

a) Fomu ya uhakiki
b) Majaribio
c) Mazoezi

### 2.2 Azimio la Kazi

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana ya Azimio la Kazi
b) Kueleza umuhimu wa Azimio la Kazi
c) Kutayarisha Azimio la Kazi la Somo la Stadi za Kazi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Onesho mbinu la namna ya kutayarisha Azimio la Kazi.
c) Majadiliano

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Sampuli za Azimio la Kazi
b) Kalenda
c) Vitabu vya rejea
d) Muhtasari wa Stadi za Kazi.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo
b) Jaribio

## 2.3 Andalio la Somo

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana ya Andalio la Somo.
b) Kuelezea umuhimu wa Andalio la Somo
c) Kueleza vipengele vya Andalio la Somo
d) Kutayarisha Andalio la Somo

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Majadiliano
c) Onesho mbinu la kutayarisha Andalio la Somo.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Sampuli za Andalio la somo
b) Muhtasari wa Stadi za Kazi.
c) Ratiba ya shule.
d) Azimio la Kazi.

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo
b) Majaribio

## 2.4 Shajara ya Somo

**Muda: Saa 1**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana ya shajara ya somo.
b) Kufafanua vipengele vya shajara ya somo
c) Kutumia shajara ya somo.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Kazi mradi kutengeneza na kutumia shajala ya somo.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

Sampuli ya Shajara ya somo

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo
b) Kazi mradi ya kupima uelewa wa mwanachuo katika kuandaa shajara ya somo la Stadi za Kazi.

## 2.5 Zana za Kufundishia na Kujifunzia

**Muda: Saa 4**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza dhana ya zana za kufundishia na kujifunzia.
b) Kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia.
c) Kutumia zana mbalimbali za kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo
b) Onyesho mbinu kuonyesha namna ya kufaragua na kutengeneza zana.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Sampuli mbalimbali za zana/vifaa vya kufundishia/kujifunzia
b) Makunzi ya aina mbalimbali

**Upimaji**

a) Mazoezi
b) Kazi mradi kuandaa zana za kufundishia na kujifunzia

# 3.0 UFUNDISHAJI WA MADA TEULE

## 3.1 Maandalizi ya Ufundishaji

**Muda: Saa 10**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kubaini mada ndogo kwa ajili ya kufundisha.
b) Kuchambua vipengele muhimu vya kuzingatia wakati wa ufundishaji.
c) Kuandaa somo la mfano.
d) Kufundisha somo la mfano.
e) Kutathmini somo na kutoa mrejesho.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Majadiliano
c) Onyesho mbinu la namna ya kufundisha.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Andalio la somo.
b) Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia
c) Muhtasari wa somo husika.
d) Azimio la kazi.

**Upimaji**

a) Majaribio
b) Mazoezi

## 3.2 Ufundishaji wa Usanii, Picha, Chapa Maumbo na Mapambo

### 3.2.1 Ufundishaji wa Usanii wa Picha kwa Rangi za Maji.

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuandaa somo la ufundishaji wa usanii wa picha kwa kutumia rangi
b) Kufundisha somo kuhusu usanii wa picha kwa rangi za maji
c) Kufanya tathmini juu ya somo la usanii wa picha kwa rangi za maji na kufanya maboresho.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Majadiliano katika vikundi
c) Onesho mbinu la kusanifu picha kwa kwa rangi za maji.
d) Matembezi ya galari.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Rangi za maji, Maji
b) Brashi, karatasi za kuchorea, vibanio au gundi ya utepe, vibao vya kuwekea karatasi wakati wa kuchora.
c) Sampuli za picha.

**Upimaji**

a) Mazoezi na majaribio
b) Kazi mradi ya kusanifu picha kwa kutumia rangi za maji.

### 3.2.2 Uchapaji kwa Njia ya Kimia

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuaridhia mbinu mbalimbali zitakazotumika kufundishia na kujifunzia somo la uchapaji kwa njia ya kimia.
b) Kuandaa somo la kuchapa kwa kutumia kimia.
c) Kufundisha somo la mfano kuhusu kuchapa kwa kutumia kimia kwa mazoezi ya kufundisha kipindi kimoja.
d) Kutathmini somo na kutoa mrejesho.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Ziara ya mafunzo kuangalia uchapaji kwa kutumia kimia
c) Onesho mbinu kuonesha namna ya kuchapa kwa kutumia kimia.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Fremu ya kimia, kisambazio cha rangi, karatasi nyeupe, stenseli, gundi ya utepe, sampuli za chapa, meza, magazeti.
b) Rangi mbalimbali

**Upimaji**

a) Mazoezi.
b) Orodha hakiki.
c) Ripoti
d) Fomu ya uchunguzi

### 3.2.3 Upambaji wa Nguo kwa Mafundo

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kuainisha mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji upambaji nguo kwa mafundo.
b) Kuandaa somo la upambaji nguo kwa njia ya mafundo.
c) Kufanya ufundishaji kiduchu kuhusu kupamba nguo kwa njia ya mafundo
d) Kutathmini somo na kutoa mrejesho.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Onesho mbinu kuonesha namna ya kupamba nguo kwa kutumia mafundo.
c) Majadiliano katika vikundi
d) Ziara ya mafunzo kuona nguo zinavyopambwa kwa kutumia mafundo.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Vitambaa vyeupe vya pamba/au vyenye rangi moja
b) Rangi za nguo, maji
c) Kamba za katani, uzi mnene, vitambaa, moto, mwiko/vijiti, kokoto, vifuniko vya soda, sufuria kubwa au pipa

**Upimaji**

a) Maswali ya mdomo
b) Mazoezi
c) Orodha hakiki.

## 3.3 Utarizi wa Mishono Mbalimbali

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji kuhusu kutambua aina mbalimbali za mishono ya kutarizi.
b) Kuandaa somo kuhusu utarizi wa mishono mbalimbali.
c) Kufanya mazoezi ya ufundishaji juu ya kuchora motifu mbalimbali.
d) Kutathmini somo na kutoa mrejesho kuhusu kutarizi mishono mbalimbali.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Onyesho mbinu kuonyesha namna ya kutarizi.
c) Majadiliano katika vikundi.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Sampuli za mishono ya kutarizi
b) Sindano za kutarizia
c) Nyuzi za rangi mbalimbali za kutarizia
d) Vitambaa vyeupe
e) Gurudumu la kutarizia.

**Upimaji**

a) Majaribio
b) Fomu ya uchunguzi
c) Orodha hakiki

## 3.4 Uigizaji

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kubaini mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji
b) Kuandaa somo kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji.
c) Kufanya ufundishaji kiduchu juu ya uigizaji matukio mbalimbali.
d) Kutathmini somo na kutoa mrejesho.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Onyesho mbinu kuonesha namna ya kuigiza hatua kwa hatua
c) Majadiliano

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Sampuli za picha za vikundi vya aina mbalimbali vya sanaa za maonesho.
b) Vifaa vitakavyohusika katika kila aina ya sanaa itakayoonyeshwa.

**Upimaji**

a) Uandishi wa insha.
b) Fomu ya uchunguzi.

## 3.5 Muziki

### 3.5.1 Uimbaji wa Solfa

**Muda: saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kuandaa somo kuhusu ufundishaji wa uimbaji wa solfa za muziki na sauti zake
b) Kufundisha uimbaji wa solfa.
c) Kutathmini somo na kutoa mrejesho.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo

b) Majadiliano

c) Onyesho mbinu la kuimba nyimbo kwa solfa

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Chati ya solfa za muziki

b) Kinanda

**Upimaji**

a) Mazoezi

b) Majaribio

c) Fomu ya uchunguzi

### 3.5.2 Upigaji Ala Sahili za Muziki

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo mwanachuo aweze:

a) Kuandaa somo kuhusu upigaji wa ala mbalimbali sahili za muziki

b) Kufanya mazoezi ya ufundishaji juu ya upigaji ala sahili za muziki

c) Kutathmini somo na kutoa mrejesho.

**Mbinu za Kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu

b) Onesho mbinu kuonyesha upigaji wa ala sahili za muziki

c) Majadiliano

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Ala mbalimbali za muziki.

b) Nyimbo zilizorekodiwa.

c) Redio kaseti

d) Seti ya televisheni

**Upimaji**

a) Mazoezi
b) Majaribio
c) Fomu ya uchunguzi

## 3.6 Kilimo na Ufugaji

### 3.6.1 Ustawishaji wa Mboga Mbalimbali

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo mwanachuo aweze:

a) Kuandaa somo kuhusu ufundishaji wa ustawishaji wa mboga wa mboga bustanini.
b) Kufanya ufundishaji wa mfano juu ya ustawishaji wa mboga mbalimbali.
c) Kutathmini somo na kutoa mrejesho

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Maonesho
c) Ziara kuona ustawishaji mboga katika bustani.
d) Onesho mbinu.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Mboga katika bustani au sampuli za picha zake.
b) Vifaa/zana za kilimo au sampuli picha zake.
c) Sampuli za dawa za mimea.

**Upimaji**

a) Maswali na majibu
b) Majaribio na mazoezi
c) Kazi mradi ya kustawisha mboga

### 3.6.2 Ufugaji Bora wa Kuku wa Kienyeji

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuainisha mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji kuhusu ufugaji kuku wa kienyeji.
b) Kuandaa somo kuhusu ufundishaji wa ufugaji bora wa kuku wa kienyeji.
c) Kufanya ufundishaji kiduchu juu ya ufugaji bora wa kuku wa kienyeji.
d) Kutathmini somo na kutoa mrejesho.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo
b) Majadiliano
c) Kazi mradi ya ufugaji wa kuku wa kienyeji

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Kuku wa kienyeji
b) Vyakula vya kuku
c) Maji safi, sampuli za picha ya mabanda ya kuku
d) Vifaa vya kulishia kuku
e) Sampuli za majedwali ya kumbukumbu za ufugaji kuku.
f) Sampuli za picha za kuku mbalimbali
g) Andalio la somo
h) Azimio la kazi.

**Upimaji**

a) Maswali na majibu
b) Fomu ya uchunguzi
c) Orodha hakiki.

## 3.7 Upishi

**Muda: Saa 4**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii ndogo, mwanachuo aweze:-

a) Kuainisha mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji upishi.
b) Kuandaa somo kuhusu upishi wa vyakula mbalimbali
c) Kufanya mazoezi ya ufundishaji kuhusu kupika vyakula mbalimbali
d) Kutathmini somo na kutoa mrejesho.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Majadiliano
c) Onesho mbinu la kupika vyakula mbalimbali

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Vyombo vya kuandalia na kuhifadhia chakula.
b) Sampuli ya vyakula mbalimbali
c) Sampuli ya vifaa vya kupikia
d) Sanduku la huduma ya kwanza
e) Kimori na kofia/kitambaa
f) Andalio la somo
g) Azimio la kazi.

**Upimaji**

a) Majaribio
b) Orodha hakiki kuchunguza ufanisi wa upishi
c) Fomu ya uchunguzi.

## 3.8 Biashara Ndogo Ndogo

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kuainisha mbinu mbalimbali za ufundishajina ujifunzaji wa biashara ndogo ndogo.
b) Kuandaa somo kuhusu ufundishaji wa biashara ndogondogo
c) Kufundisha somo la mfano shule ya jirani kuhusu biashara ndogo ndogo
d) Kutathmini somo na kutoa mrejesho.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Majadiliano
b) Igizo dhima kuonyesha namna ya kufanya biashara ndogo ndogo.
c) Ziara ya mafunzo kuona jinsi biashara ndogo ndogo zinavyofanywa.
d) Maswali na majibu.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Sampuli picha za maeneo ya biashara
b) Sampuli za bidhaa mbalimbali
c) Picha za aina mbalimbali za biashara ndogondogo.
d) Leseni
e) Mchanganuo wa biashara.
f) Andalio la somo
g) Azimio la kazi.

**Upimaji**

a) Mazoezi au majaribio
b) Majaribio na mazoezi
c) Fomu ya uchunguzi.

### 3.9 Ufundi

#### 3.9.1 Matengenezo ya Baiskeli

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:

a) Kuandaa somo kuhusu matengenezo ya baiskeli.
b) Kufundisha kiduchu namna ya kufanya matengenezo ya baiskeli.
c) Kutathmini somo na kutoa mrejesho kuhusu kufanya matengenezo ya baiskeli

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Kualika mtaalamu kuongoza namna ya kufanya matengenezo ya baiskeli.
c) Onesho mbinu
d) Majadiliano katika vikundi.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Spana, bisibisi, nyundo, grisi, dawa ya kuzibia pancha.
b) Baiskeli iliyoharibika
c) Chati yenye michoro ya sehemu za baiskeli.
d) Andalio la somo na maazimio ya kazi

**Upimaji**

a) Maswali na majibu
b) Mazoezi
c) Orodha hakiki

#### 3.9.2 Matengenezo ya Viatu

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kuainisha mbinu mbalimbali kuhusu ufundishaji na ujifunzaji matengenezo ya viatu
b) Kuandaa somo kuhusu ufundishaji wa kufanya matengenezo ya viatu
c) Kufanya mazoezi ya kufundisha matengenezo ya viatu kipindi kimoja.
d) Kutathmini somo na kutoa mrejesho kuhusu somo la matengenezo ya viatu.

**Mbinu za Kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Majadiliano
c) Ziara katika kufundisha juu ya matengenezo ya viatu.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Viatu
b) Vifaa vya kushonea viatu kama uzi wa kushonea viatu, sindano, vipande vya ngozi, gundi ya viatu, nyundo, misumari, kisuwembe, nta, soli ya kiatu sabuni na lasti.

**Upimaji**

a) Mazoezi na majaribio
b) Orodha hakiki kuhusu ufundishaji wa utengenezaji wa viatu

.

## 3.10 Upigaji Picha Tuli

**Muda: Saa 2**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze

a) Kubainisha mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji kuhusu kupiga picha tuli.
b) Kuandaa somo kuhusu ufundishaji wa upigaji picha tuli.
c) Kufanya ufundishaji wa somo la mfano kuhusu upigaji picha tuli.
d) Kutathmini somo na kutoa mrejesho kuhusu upigaji picha tuli.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo

b) Onesho mbinu.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Kamera

b) Sampuli za picha mbalimbali

c) Chati ya orodha ya kanuni za upigaji picha.

**Upimaji**

a) Mazoezi

b) Fomu ya uchunguzi

c) Ripoti

## 4.0 UPIMAJI

### 4.1 Dhana ya Upimaji

**Muda: Saa 1**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii mwanachuo aweze:

a) Kueleza maana ya upimaji.

b) Kuainisha upimaji

c) Kufafanua umuhimu wa upimaji

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali na majibu

b) Majadiliano

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali

b) Majaribio

c) Mitihani

d) Uchunguzi
e) Kazi mradi
f) Mkoba wa kazi
g) Orodha hakiki

**Upimaji**

Insha kuhusu dhana ya upimaji

## 4.2 Uandaaji na Utunzaji wa Zana za Upimaji

**Muda: Saa 3**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada hii, mwanachuo aweze:

a) Kuaridhia aina za zana za upimaji
b) Kueleza umuhimu wa zana za upimaji
c) Kuandaa zana mbalimbali za upimaji
d) Kutunza Zana za Upimaji

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Fikiri jozisha shirikisha
b) Onyesho mbinu kuhusu namna ya kuandaa zana za upimaji

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

Sampuli za zana za upimaji

**Upimaji**

a) Majaribio
b) Mkoba wa kazi

## 4.3 Matokeo ya Upimaji

**Muda: Saa 1**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza umuhimu wa matokeo ya upimaji
b) Kutathmini matokeo ya upimaji
c) Kueleza jinsi atakavyotumia matokeo ya upimaji

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Majadiliano
c) Bungua bongo

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

Matokeo ya upimaji

**Upimaji**

Mazoezi na majaribio

## 4.4 Utunzaji wa kumbukumbu za upimaji

**Muda: Saa 1**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:

a) Kueleza umuhimu wa kutunza kumbukumbu za upimaji
b) Kufafanua hasara za kutotunza matokeo ya upimaji
c) Kuonyesha namna atakavyotunza kumbukumbu za matokeo ya upimaji

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Maswali na majibu
b) Onyesho mbinu kuonyesha namna ya kuweka kumbukumbu za upimaji.

**Vifaa/zana za kufundishia na kujifunzia**

a) Sampuli za kumbukumbu matokeo ya upimaji zilizohifadhiwa

b) Nyenzo za kuhifadhia kumbukumbu za upimaji

**Upimaji**

Mazoezi na majaribio

**REJEA**

Wizara ya Elimu na Utamaduni (2003) Muhtasari wa Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti – Mbinu za Kufundishia/Kujifunzia somo la Stadi za Kazi – Wizara ya Elimu na Utamaduni, DSM.

Wizara ya Elimu na Utamaduni, (2005) Muhtasari wa Stadi za Kazi kwa shule za Msingi, Wizara ya Elimu na Utamaduni DSM.

Wizara ya Elimu na Utamaduni (2005) Mpango wa Mafunzo ya Walimu Kazini-Darajani la IIIC/B – IIIA – Moduili ya Somo la Stadi za Kazi – Somo la I, Wizara ya Elimu na Utamaduni, DSM.

Wizara ya Elimu na Utamaduni (2005) Mpango wa Mafuzo ya Walimu Kazini Daraja la IIIC/B – IIIA – Moduli ya somo la Stadi za Kazi, somo la 3, DSM.

Tanzania Insititute of Education 2008 Guide for Teaching Vocational Skills in Primary Schools in Tanzania, Tanzania Institute of Education, DSM.

Ministry of Education and Culture (2005) Music Syllabus for Secondary Schools, Form I – IV, Mnistry of Education and Culture, DSM.

Ministry of Educational and Culture (2005) Fine Arts Syllabus for Secondary Schools Form I – IV, Ministry of Education and Culture, DSM.